**JESMA 004**

# JARIBIO LA NNE K.C.P.E
# DARASA LA NANE

**KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

## SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

## JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Mtu anayetengeneza vyombo vya vyuma ni

A. sonara
B. rubani
C. mhunzi
D. mwashi

Jibu sahihi ni C

**1** [A] [B] [C] [D] **11** [A] [B] [C] [D] **21** [A] [B] [C] [D] **31** [A] [B] [C] [D] **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**



FUNGUA UKURASA

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Msimu wa mvua ya masika ____**1**____, wakulima huwa tayari ____**2**____ makonde yao kwa upanzi. Siku chache baada ya mvua ____**3**____ kuanza, mbegu huanza ____**4**____ na kunawiri. ____**5**____ kunyesha kwa mvua ____**6**____ huja na madhara yake pia. Maji yaliyotuama huwawezesha mbu kuzaana kwa wingi. Halikadhalika maji haya husomba taka kutoka kila mahali. Matokeo ya hali hii huwa na mlipuko wa maradhi kama ____**7**____ . Mvua ambayo kwa kawaida____**8**____ baraka huleta baa chungu nzima. Janga la njaa huwa ____**9**____ macho.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. yanapowadia | B. inapowadia | C. unapowadia | D. inayowadia |
| **2.** | A. wameiandaa | B. wameziandaa | C. wameuandaa | D. wameyaandaa |
| **3.** | A. yenyewe | B. wenyewe | C. zenyewe | D. mwenyewe |
| **4.** | A. kustawi | B. kuchipuka | C. kukomaa | D. kupogoa |
| **5.** | A. Ila | B. Ingawa | C. Angalau | D. Lakini |
| **6.** | A. kiholela | B. kivoloya | C. kidindia | D. kwa haraka |
| **7.** | A. waba, kichocho na malaria | B. malale, kichocho na mkamba | C. homa, kichocho na surua | D. malaria, kisonono na kipindupindu |
| **8.** | A. imekuwa | B. ilikuwa | C. inakuwa | D. ingekuwa |
| **9.** | A. imewaangazia | B. limewakodolea | C. imewakodolea | D. inawaangalia |

Mwanadamu anapaswa kuwa na ____**10**____ maishani; aelewe ____**11**____ utotoni ni mambo yapi hasa angependa kutimiza kabla ya kula chumvi. Akishayajua haya, basi hana budi kuanza kujiwekea ____**12**____ kuyafikia haya. Bidii pia ni muhimu sana maishani. Wahenga walituasa kuwa ____**13**____. Tusikae ____**14**____ na kuyangoja maisha kujipitia ____**15**____ mkondo wa maji.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. ndweo | B. matayo | C. malengo | D. upweke |
| **11.** | A. tangu | B. hadi | C. mpaka | D. kabla |
| **12.** | A. stadi za | B. mikakati ya | C. ujuzi ya | D. mwelekeo ya |
| **13.** | A. penye nia pana njia | B. ushikwapo shikamana | C. dhamira ni dira | D. ajizi ni nyumba ya njaa |
| **14.** | A. ugeta | B. kitwea | C. ange | D. tutwe |
| **15.** | A. mithili wa | B. mfano ya | C. mithili ya | D. mathalani wa |

*Kuanzia swali la* **16** *hadi* **30**, *jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Tambua orodha inayoangazia nomino za jumla pekee.
A. maji, maziwa, mchanga, unga
B. watoto, nyumba, kabati, meza
C. woga, wivu, furaha, hofu
D. bumba, kigaro, genge, halaiki

**17.** Ni sentensi gani iliyotumia kihusishi '**kwa**' kuonyesha sababu ya kutenda jambo?
A. Nimealikwa sherehеni kwa Maria
B. Alinijibu swali hilo kwa dharau
C. Halima anapendwa kwa utulivu wake
D. Baba alikuja mkutanoni kwa baiskeli

**18.** Maelezo yapi ni sahihi kuhusu ufundi?
A. Timazi hutumiwa kupimia usawa wa ukuta
B. Jiriwa hutumiwa kufungia parafujo
C. Mizani hutumiwa kupimia urefu
D. Filifili hutumiwa kushikia ubao unapokatwa

**19.** Tegua kitendawili kufuatacho:
Nimemwona bikizee amejitwika machicha
A. samaki
B. mvi
C. ajuza
D. mnazi

**20.** Nahau ipi ina maana ya kupata tabu?
A. Kula mwande
B. Enda nguu
C. Enda mserego
D. Kula mwata

**21.** Jumla ya silabi katika mshororo wa shairi ni
A. vina
B. inkisari
C. mizani
D. mazida

**22.** Kamilisha kwa kiulizi kifaacho zaidi
Unataka nikusaidie ____________?
A. aje
B. pi
C. je
D. vije

**23.** Tabia ya kuongeza yasiyo ya kweli ili kutilia mkazo katika habari fulani huitwa________.
A. chuku B. tasfida
C. sitiari D. kejeli

**24.** Ainisha maneno yaliyokolezwa wino katika sentensi ifuatayo.
Haijulikani mtoto **huyo** alienda **wapi**.
A. Kiashiria, kiwakilishi
B. Kiwakilishi, kielezi
C. Kiwakilishi, kiulizi
D. Kivumishi, kielezi

**25.** Ukitaka watu wakupishe njia utawaambia
A. makiwa B. simile
C. kunradhi D. hebu

**26.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo:
Fundi mzuri amenikarabatia redio yangu
A. Fundi wazuri wamenikarabatia redio zangu
B. Mafundi mazuri yametukarabatia redio zetu
C. Fundi wazuri wametukarabatia maredio yetu
D. Mafundi wazuri wametukarabatia redio zetu

**27.** Neno **mkeka** lina sauti ngapi?
A. Mbili B. Tatu
C. Tano D. Nne

**28.** **Mtu akipatwa na tatizo huwa sio mwisho wake kwani muda mfupi atalitatua na kuendelea.** Jumuisha ujumbe huu kwa methali
A. Kuteleza sio kuanguka
B. Baada ya kisa mkasa
C. Kuunguako ndiko kuteketeako
D. Kuti kavu kuanguka si ajabu

**29.** Kati ya ala zifuatazo, ipi ni ya kupuliza?
A. Fidla B. Zumari
C. Udi D. Marimba

**30.** Ungo ni gamba la kaa. Ungo pia ni
A. kubalegh kwa wasichana
B. vumbi la kitu kilichosagwa
C. habari isiyo ya kweli
D. kifaa cha kupepeta nafaka

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* **31 – 40**

Bwana Toza alikuwa mkaramfu, hivyo hulka yake ilihusudiwa na mabarubaru wengi. Ila falau wangalijua kuchuja, wangeiga yaliyo mema kama mbinu zake za kuzalisha mali zisikowa na ila na kuyatema yasiyofaa. Ilikuwa si ajabu kuwaona wakembe wengi wakitia mirija kwenye mikebe wakaishidilia tumbaku na kuzivuta 'toza' zao kama Bwana Toza. Kwa kufanya hivyo walijihisi, eti wamefikia upeo wa kunasibishwa na Bwana Toza aliyetosha! Wakaamini kuwa maadamu toza zilitoka ulaya na wakazi wa huko wana maendeleo makuu, basi kila aivutaye hatimaye angepata ufanisi. Hii ni imani ya ajabu inayowakabili hirimu - kuiga, kikasuku. Mzungu akija na miondoko ya kikwao, humwiga wakidhani huo ndio ustaarabu hasa.

Siku zilivyozidi kupita, Bwana Toza akawaambukiza insi wengi uvutaji wa toza akajiona kama mflame aliyetawala himaya nzima ya wavuta mitemba. **Wengine waliianza tabia hii kidogo kidogo lakini baada ya muda wakakolewa nayo wakawa watumwa.** Waliokuwa wakiivutia maliwatoni, sasa wakaivuta hadharani, wakatafuta viko hasa ili wainue hadhi zao maadamu wanasibishwe na Bwana Toza. Akawa ambari nao zinduna.

Azima ya kufikia kilele huwafanya wakwasi kutafuta sifa. Bwana Toza akang'amua kuwa sasa ana wafuasi tosha. Kwa hivyo akaona kuwa lau angekiwania kiti cha ubunge cha eneo la kwao, angejinyakulia kiti hicho bila shida. Uchaguzi ulipotangazwa, akajitwika mzigo wa kugaragazana na wawaniaji wengine. Akawakusanya wafuasi wake wa tozani. Kwa moyo na roho moja, wakashauriana kuhusu jinsi ya kuwakabili wapinzani wao.

Ukawa ndio mwanzo mkoko ualike maua. Alama ya chama chao ikawa kiko. Basi katika mikutano ya kampeni wakaviwasha viko vyao na huku vyafuka moshi wangeviinua na kupasua hewa kukinadi chama chao.

Mara kwa mara Bwana Toza alizoea kuamka bukrata ila mara nyingi alijihisi kuwa amechoka tiki na kuregea parafujo za mwili, kutokana na mavune ya kampeni na mtindi aliopiga kila uchao.

Siku moja karibu na mwisho wa majira ya kampeni, Bwana Toza alifika kuwahutubia wafuasi wake waliokuwa wameongezeka kupita kiasi. Alikuwa bado hajapata nafuu. Hata hivyo alijikakamua kwa shida, huku akikohoakohoa. Huku mkono watetema alisema, 'kikoo!' Halaiki ikajibu kwa mwangwi 'kikooo--o! 'Mara ya pili akajaribu kusema, 'kik-oho--ho--kho--kho--'

Badala ya kiko kikawa kikohozi kisichopoa. Hakuendelea. <u>Akaanguka kifudifudi</u>. Wafuasi wake wakamkimbilia na kugundua kuwa alikuwa amepaliwa na pumzi. Wakajaribu maarifa yote ya huduma ya kwanza. walimvuvia, wakampepesa, wakambinyabinya kifua lakini wapi! Jitihada za kuinusuru aushi ya Bwana Toza kitambo kile. Mambo yote yakafikia hatima ya ghafla.

Upasusi ulipofanywa ulionyesha kuwa Bwana Toza alimalizwa na toza. Pafu lilikuwa jeusi kama kaa lilininginiwa na masizi mengi ajabu. Ripoti hii iliposomwa mbele ya wafuasi wake, wakaduwaa macho pima. Mitemba ikaanza kuwadondoka kutoka midomoni mmoja mmoja.

**31.** Chagua kauli sahihi kulingana na aya ya kwanza:

A. Sifa za Bwana Toza ziliwavutia vijana wote
B. BwanaToza alikuwa mtu wa furaha
C. Bwana Toza alijipatia mali kwa njia haramu
D. Mambo yote ya Bwana Toza yalifaa

**32.** Wakembe walitia mirija kwenye mikebe

A. ili wapate viko vya kuvutia tumbaku
B. kwa maelekezo ya Bwana Toza
C. kwa kuogopa kushika vikoa halisi
D. ili wajilinganishe na Bwana Toza

**33.** Kosa kubwa la vijana kulingana na makala ni

A. kupuuza ustaarabu wao na kuiga hata yasiyofaa
B. kuiga ustaarabu wa kigeni pamoja na wa kwao
C. kuvutiwa na maendeleo ya nchi za ulaya
D. kuvuta viko vilivyotengenezewa ulaya

**34.** **'Wengine waliianzia tabia hii kidogo kidogo lakini baada ya muda wakakolewa nayo wakawa watumwa'** Ni methali gani inayoambatana na kauli hii?

A. Anayeonja asali huchonga mzinga.
B. Abadi abadi kamba hukata jiwe.
C. Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma.
D. Mwanzo wa ngoma ni lele.

**35.** Kilichomfanya Bwana Toza kujitosa katika ulingo wa siasa ni

A. kujitafutia sifa zaidi
B. kujitafutia kipato zaidi
C. kupata wafuasi zaidi
D. kusumbuliwa na pesa

**36.** Alama ya chama cha Bwana Toza ilikuwa

A. sigara
B. mtemba
C. mrija
D. vidole

**37.** Uchovu wa Bwana Toza ulichangiwa na

A. ugonjwa na kampeni
B. uzee na ulevi
C. uchovu na ulevi
D. uchovu na kuamka mapema

**38.** Maana ya '**kuanguka kifudifudi**' ni

A. kuangukia mgongo
B. kuanguka bila hiari
C. kuanguka kwa kishindo
D. kuangukia tumbo

**39.** Wafuasi walipojuzwa kuhusu chanzo cha mauti ya Bwana Toza

A. walipigwa na butwaa
B. walichanganyikiwa sana
C. waliogopa sana
D. walipiga kamsa

**40.** Kichwa mwafaka kwa makala haya ni

A. Madhara ya ulevi
B. Kifo cha mtu wa watu
C. Madhara ya tumbaku
D. Mbio za sakafuni huishia ukingoni

*Yasoma makala haya kisha ujibu maswali* **41 – 50**

Adinasi walio na kasoro ya macho, miguu, masikio na kadhalika, ambao kwa bahati mbaya tunawaita vipofu, viwete na viziwi. Kwa kukosa majina bora zaidi, wanahitaji macho, miguu, masikio na hata mikono yetu. Ni mara ngapi watu hao wamekosa watu wa kuwaongoza kuvuka barabarani au hata gurufuni? Mara ngapi watu waliolemaa miguu wameachwa tu waozee mahali pamoja bila kupata mtu wa kuwageuza hata waliapo kwa uchovu na maumivu? Ni mara ngapi wamekosa wa kuwapeleka watakapo; wengine hata kunyimwa viti vya magurudumu hata vipatikanapo?

Kijumla, hasa katika Janibu za Afrika, wengi wanaowapata watoto waatilifu hudhani wamechomekwa mizizi au kuapizwa na wazee wao waliowatangulia. Huku wakiwaonea gere waliopata wana buheri wa hamsa wa ishirini si ajabu kusikia kuwa mtoto alizaliwa miaka kadhaa iliyopita na kufichwa hata mvunguni mwa kitanda katika chumba kilichofichama. Si ajabu pia kuwaona watu kama hawa wakienda vilingeni kupungiwa wanao. Utawaona wakwasi wenye mashamba madal basari, mapana kama uwanja wa ahera wenye matumbo kama viriba na waendeshao magari ya kifahari wakiingia vilingeni

mali mengi na mwanawe asipone, hali hii huzidisha tu dhuluma kwa muatilifu kwa kuwa sasa huonekana kama mjalaana.

Watoto waatilifu pia hubaguliwa kimasomo. Sijui aliyefichwa mvunguni atapata elimu lini? Vipi? Wao huchukuliwa eti kasoro waonekanazo nazo zitawakwaza masomoni. Hata serikali ikijaribu kuwatengenezea shule maalum, bado kunao wanaowanyima wanao nafasi hii bila kujua kuwa Maulana humnyima huyu hiki na kumpa kile. Kuwanyima fursa ya kuvitambua vipawa vyao ni dhuluma isiyomithilika.

Ajabu ni kuwa, waatilifu wakomaapo, wengi hukaa bila kupata wa kuwaoa au kuoa licha ya juhudi zao za kujimudu kiuchumi na kijamii. Wengi huchelea kubezwa eti wameoa 'wasiojiweza'. Jitihada za wengi kuwaoa watilifu zimevuliwa mbeleko na watu wa familia zao.

Kuchekwa kukebehiwa na kudharauliwa huwaletea simanzi waatilifu hawa na hujiona kama kizazi kisicho na thamani. Na ni nani aliyechagua au kuamua kuzaliwa katika hali aliyo kwayo? Ni nani aliyesema kuwa tusio na uatilifu ulio dhahiri tumekamilika? Je tukichunguzwa kila mmoja wetu upungufu tulio nao kisha tudhulumiwe tutateta? Aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi. Waidha, mdharau biu hubiuka yeye.

**41.** Mwandishi anaonekana kutokubaliana na

A. majina mbalimbali wanayoitwa walemavu
B. hali ya watu kupata ulemavu mbalimbali
C. kuwa yapo mambo wasiyoyaweza waatilifu
D. walemavu wanahitaji msaada wa wazima

**42.** Kukosa kumsaidia mlemavu kuvuka njia ni ukosefu wa

A. uzalendo
B. huruma
C. amani
D. upole

**43.** <u>Gurufu</u> kulingana na makala ni

A. barabara yenye kuruba nyingi
B. barabara pana za mijini
C. baraste isiyo na shughuli nyingi
D. barabara yenye magari mengi

**44.** Njia bora zaidi ya kuwaauni watu wenye ulemavu ni

A. kuwapeleka kila mahali wanapotaka
B. kuwanunulia chochote wanachohitaji
C. kuwaongoza kuvumbua namna ya kujikimu
D. kuwahurumia kutokana na maumbile yao

**45.** Kauli gani **SI** sahihi kuhusu mitazamo ya ulemavu barani Africa?

A. Ulemavu husababishwa na laana ya wazee
B. Uatilifu hutokana na kurogwa na wenye nia mbaya
C. Uatilifu humalizwa kwa uganga wa kienyenji
D. Ulemavu ni jambo la kudura tu

**46.** Zifuatazo ni ishara za ukwasi zilizoangaziwa kwenye makala haya ila

A. tumbo kubwa lililoshuka
B. makonde makubwa
C. kumiliki magari mengi
D. magari ya kifahari

**47.** Manufaa ya elimu kulingana na mwandishi ni

A. utambuzi wa vipawa
B. kutimiza haki za watoto
C. kujipatia ajira nzuri
D. kuyatawala mazingira

**48.** Watu hawapendi kuwaoa au kuolewa na walemavu kwa

A. kuogopa majukumu
B. kuhofia kudharauliwa
C. kuwaona kama kinyaa
D. kutowaona kama binadamu

**49.** Mtu asiyeweza kusikia huitwa

A. bubu
B. toinyo
C. kibunye
D. kiduko

**50.** Msimamo wa mwandishi katika aya ya mwisho ni kuwa

A. Mungu pekee ndiye mpaji na mtoaji wa yote tuliyo nayo
B. Kila mmoja wetu ana kasoro za walemavu
C. Familia ni kikwazo katika ndoa za walemavu
D. Wanyonge wanapodharauliwa huwa hawana thamani tena